# HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI MHESHIMIWA RAHMA KASSIM ALI (MBM) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

## UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** kwa ruhusa yako, naomba kuwasilisha Hotuba ya bajeti ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kazi za Kawaida na Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi.

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, naomba nichukuwe nafasi hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) Mwingi wa Rehema kwa kutujaalia afya njema, uwezo na nguvu za kutekeleza yale yote tuliyojipangia katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. Vile vile, kwa rehema za Mwenyezi Mungu Mtukufu ametuwezesha kukutana hapa leo tukiwa katika hali ya usalama, amani na

utulivu katika uwasilishaji wa hotuba ya bajeti ya Wizara hii mbele ya Baraza lako Tukufu.

3. **Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Viongozi na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, napenda kuchukua nafasi hii adhimu kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri iliyotukuka anayoifanya katika kuwaletea Maendeleo Wananchi wa Tanzania kwa ujumla kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 - 2025.

4. **Mheshimiwa Spika,** vilevile, kwa udhati kabisa naomba kuchukuwa fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa ufuatiliaji makini wa utendaji uliotukuka wa Serikali anayoiongoza. Tunampongeza na kumshukuru zaidi kwa miongozo mbali mbali anayotupatia katika kuhakikisha kwamba Wizara na Taasisi zetu zinatoa

huduma bora kwa Wananchi na kwa wakati muafaka.

5. **Mheshimiwa Spika,** aidha, natoa shukrani kwa Makamo wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamo wa Pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa jitihada wanazofanya katika kumsadia Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Jitihada hizo ni pamoja na ufuatiliaji wa kazi zinazotekelezwa na Serikali na Uhamasishaji wa Amani, Umoja na Mshikamano.

6. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee, napenda kukupongeza wewe binafsi pamoja na Naibu Spika na wasaidizi wako kwa busara na hekima mnazozitumia katika kuliongoza Baraza hili. Aidha, naomba kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Yahya Rashid Abdallah kwa Ushirikiano, Ushauri na Maelekezo mbali mbali ambayo wamekuwa wakitupatia katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu.

7. **Mheshimiwa Spika,** naomba pia kutoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Mheshimiwa Nadir Abdullatif Yussuf Alwardy kwa ushirikiano wake mkubwa anaonipa katika kuiongoza Wizara hii. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu kwa Katibu Mkuu Ndugu Joseph John Kilangi, Wakuu wa Taasisi pamoja na Watendaji na wafanyakazi wote wa Wizara hii ambao kwa pamoja wamenipa Ushirikiano wao wa hali ya juu katika kuongoza na kutekeleza majukumu ya Wizara na kuhakikisha kwamba Wananchi wa Zanzibar wanafaidika na huduma muhimu zinazotolewa na Wizara yangu.

8. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kimuundo inajumuisha Idara na Taasisi zake kama zinavyoonekana katika ukurasa wa nne wa hotuba yangu.

9. **Mheshimiwa Spika,** baada ya utangulizi huo naomba sasa uniruhusu kuelezea utekelezaji wa kazi za Kawaida na za

Maendeleo za Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Muelekeo wa Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA KAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022.

10. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa utekelezaji wa shughuli za Wizara, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wizara yangu ilifanikiwa kutekeleza majukumu yake kupitia Programu kuu tatu zifuatazo:-

    a. **Programu PN0201:** Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi.

    b. **Programu PN0202:** Usimamizi wa Ardhi.

    c. **Programu PN0203:** Maendeleo ya Makaazi.

## PROGRAMU KUU PN0201: UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ARDHI

11. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina jukumu la kuimarisha uratibu katika utekelezaji wa kazi za Wizara ambayo inajumuisha programu ndogo tatu ambazo zinatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Uendeshaji na Utumishi na Afisi Kuu Pemba. Kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 utekelezaji wa programu hii ni kama ifuatavyo: -

### PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

12. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mipango Sera na Utafiti inajukumu la kuratibu na kusimamia utayarishaji wa Mipango ya Taasisi zote zilizomo ndani ya Wizara ikiwemo Sera, Sheria na Bajeti. Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Programu hii ndogo ililenga kutekeleza shughuli za uratibu na uandaaji wa Mipango na Miongozo ya Kisera ya utekelezaji wa kazi za Wizara, kuratibu uandaaji wa mapitio ya

sheria, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, kuendeleza tafiti kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa huduma pamoja na kuratibu vikao mbalimbali vya mashirikiano baina ya SMT na SMZ.

13. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi wa Machi 2022 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo:
    i. Uratibu na uandaaji wa mipango ya Wizara
    ii. Kusimamia maandalizi na utekelezaji wa Sera za Wizara na kuratibu mapitio ya Sheria
    iii. Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mipango ya Sekta
    iv. Kuimarisha Uhusiano baina ya Wizara za SMZ na SMT

14. **Mheshimiwa Spika,** maelezo ya utekelezaji wa kazi hizi ni kama inavyoonekana katika ukurasa wa 7 hadi wa 12 wa hotuba yangu.

15. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, jumla ya **TZS Milioni**

**305.4** ziliidhinishwa kutumika kwa utekelezaji wa Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti. Hadi kufikia Machi, 2022, fedha zilizopatikana ni **TZS Milioni 184.97** sawa na **asilimia 60.57** na **asilimia 80** kwa ulinganisho wa fedha zilizopangwa miezi tisa (9).

**PROGRAMU NDOGO YA UTAWALA NA UENDESHAJI**

16. **Mheshimiwa Spika,** lengo la Programu hii ni kusimamia uendeshaji wa shughuli za kila siku za Wizara pamoja na usimamizi wa rasilimali watu kwa kuandaa mipango ya kuwajengea uwezo wa Watumishi, kuimarisha mazingira bora ya kazi, kushughulikia haki na stahiki za Watumishi, kuhakikisha kuwepo kwa watendaji wa kutosha na wenye sifa pamoja na kusimamia nidhamu kwa watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake zote.

17. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza majukumu yake ya msingi Idara ya

Uendeshaji na Utumishi hadi kufikia Machi, 2022 imetekeleza kazi zake kama inavyoonekana katika ukurasa wa 13 hadi wa 14 wa hotuba yangu.

18. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2021//2022, Programu hii iliidhinishiwa jumla ya **TZS Bilioni 1.928** kwa ajili ya kufanikisha shughuli za Uendeshaji na mishahara. Hadi kufikia Machi, 2022 fedha zilizopatikana ni **TZS Bilioni 1.401** sawa na **asilimia 73** na **asilimia 93.63** kwa mlinganisho wa fedha zilizopangwa kwa miezi tisa (9).

**PROGRAMU NDOGO YA URATIBU NA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA WIZARA PEMBA**

19. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ndogo inatekelezwa na Afisi Kuu Pemba na inajukumu la kuratibu na kusimamia Utawala na Mipango ya kazi za Wizara zinazotekelezwa Pemba ikiwemo Programu na Miradi ya Maendeleo.

20. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi, 2022 programu hii ndogo imetekeleza kazi zake kama inavyoonekana katika ukurasa wa 15 hadi wa 16 wa hotuba yangu.

21. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Afisi Kuu Pemba imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 20.0.** Hadi kufikia Machi, 2022 jumla ya **TZS Milioni 11.548** zimekusanywa sawa na **asilimia 57.7** ya makadirio ya mwaka.

Kwa upande wa Matumizi Afisi Kuu Pemba ilipangiwa kutumia jumla ya **TZS Milioni 746.6,** kati ya fedha hizo **TZS Milioni 175** ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida (OC) na **TZS Milioni 571.6** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara ya wafanyakazi. Hadi kufikia mwezi Machi, 2022 fedha zilizopatikana ni Jumla ya **TZS Milioni 468.8** ambazo sawa na **asilimia 62.7** na **asilimia 82.8** Kwa ulinganisho wa fedha zilizopangwa kwa miezi tisa (9).

**PROGRAMU KUU PN0202: USIMAMIZI WA ARDHI**

22. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina jukumu la kuhakikisha usalama wa matumizi ya ardhi na umiliki (Security of Land Tenure) kwa Wananchi na imegawika katika Programu ndogo kama ifuatavyo:-

**PROGRAMU NDOGO YA USIMAMIZI WA ARDHI**

23. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2021/2022 Programu hii ililenga kutekeleza shughuli zote inazohusiana na masuala ya ardhi. Programu hii ndogo inatekelezwa na Taasisi zifuatazo: -

**MAHAKAMA YA ARDHI**

24. **Mheshimiwa Spika,** Mahakama ya ardhi imeanzishwa chini ya Sheria namba 7 ya mwaka 1994. Lengo la kuanzishwa kwake ni kupokea, kusikiliza na kuzitolea maamuzi kesi zinazotokana na migogoro ya ardhi zinazowasilishwa na Wananchi pamoja na Taasisi mbalimbali.

**25.** **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi, 2022 Mahakama ya Ardhi imetekeleza kazi zake kama zinavyoonekana katika ukurasa wa 18 hadi wa 19 wa hotuba yangu.

**26.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2021//2022 Mahakama ya Ardhi ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 7.0** ambapo hadi kufikia Machi, 2022 ilifanikiwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 6. 901** sawa na **asilimia 99** ya makadirio.

Kwa upande wa Matumizi Mahakama ya Ardhi ilipangiwa jumla ya **TZS Millioni 583.82** kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii. Hadi kufikia Machi, 2022 fedha zilizopatikana ni **TZS Milioni 377.33** sawa na **asilimia 64.6** na **asilimia 83.9** kwa mlinganisho wa fedha zilizopangwa kwa miezi tisa (9).

**OFISI YA MTHAMINI MKUU WA SERIKALI**

**27.** **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali imeanzishwa kwa Sheria

namba 5 ya mwaka 2015 kwa dhumuni la kuhakikisha usimamizi mzuri wa uthaminishaji mali kwa malengo mbalimbali ya Sekta ya umma, Biashara na Wananchi kwa ujumla. Kazi kuu ya Mthamini Mkuu ni kuthibitisha kazi za uthamini zinazofanywa nchini na Wathamini wa Taasisi za Serikali na Taasisi binafsi.

28. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali imetekeleza kazi kama inavyoonekana katika ukurasa wa 21 wa hotuba yangu.

29. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 50.0** ambapo hadi kufikia Machi, 2022 ilifanikiwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 132.392** sawa na **asilimia 265** ya makadirio.

Kwa Upande wa Matumizi Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali ilipangiwa kutumia jumla ya **TZS Milioni 151.8.** Hadi kufikia Machi, 2022 fedha zilizopatikana ni **TZS**

**Milioni 55.060** sawa na **asilimia 36.27** ya makadirio na **asilimia 48.36** ulinganisho wa fedha zilizopangwa miezi tisa (9).

**KAMISHENI YA ARDHI**

30. **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Ardhi imeanzishwa kwa Sheria Namba 6 ya Mwaka 2015. Lengo la kuazishwa kwake ni kuleta ufanisi zaidi katika kusimamia Sheria za Sekta ya ardhi pamoja na kuziunganisha Idara zote zinazosimamia matumizi na maendeleo ya ardhi.

31. **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Ardhi kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 imetekeleza kazi zifuatazo:-
    i. Ugawaji na usimamizi wa ardhi.
    ii. Kuratibu na kusimamia usajili wa ardhi.
    iii. Upimaji na utoaji wa ramani za ardhi
    iv. Upangaji wa miji na matumizi ya ardhi

32. **Mheshimiwa Spika,** maelezo zaidi ya utekelezaji wa kazi hizo ni kama inavyoonekana katika ukurasa wa 23 hadi wa 25 wa hotuba yangu.

33. **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Ardhi ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 830** ambapo hadi kufikia Machi, 2022 ilifanikiwa kukusanya jumla ya **TZS 638.059** sawa na **asilimia 77** ya makadirio.

Kwa upande wa matumizi, Kamisheni ya Ardhi ilikadiriwa kutumia jumla ya **TZS Bilioni 2.632** kwa kazi za kawaida na mishahara ambapo jumla ya **TZS Milioni 985.2** ni ruzuku ya kazi za kawaida na **TZS Bilioni 1.647** ni ruzuku ya mishahara. Hadi kufikia Machi, 2022 fedha zilizopatikana ni **TZS Bilioni 1.499** sawa na **asilimia 56.96** kwa mwaka na **asilimia 73.58** ulinganisho wa fedha zilizopangwa miezi tisa (9).

## BODI YA UHAULISHAJI ARDHI

34. **Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Uhaulishaji Ardhi imeanzishwa kwa Sheria namba 8 ya mwaka 1994. Lengo la kuanzishwa bodi hii ni kupokea na kujadili maombi ya uhaulishaji wa ardhi na baadae kutayarisha cheti cha Uhaulishaji.

35. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Bodi ya Uhaulishaji imetekeleza kazi zake kama zinavyooneka katika ukurasa wa 26 wa hotuba yangu.

36. **Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Uhaulishaji Ardhi ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS. Bilioni 3.00** hadi kufikia Machi, 2022 imefanikiwa kukusanya jumla ya **TZS. Bilioni 1.7** sawa na **asilimia 61** ya makadirio.

    Kwa upande wa matumizi Bodi ya Uhaulishaji ilikadiriwa kutumia jumla ya **TZS Milioni 850** kwa kazi za kawaida hadi kufikia Machi, 2022 imetumia jumla ya **TZS Milioni 115** sawa na **asilimia 13.5** na **asilimia 18** ya ulinganisho wa fedha zilizopangwa kwa miezi tisa (9).

**PROGRAMU KUU PN0203: MAENDELEO YA MAKAAZI**

37. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa makaazi salama na endelevu kwa wananchi

na watumishi wa Serikali, pamoja na kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji wa sekta binafsi katika huduma ya makaazi.

Programu hii inasimamiwa na Wakala wa Majengo, Shirika la Nyumba, Bodi ya Kondominio, Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba, Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo na Bodi ya Usajili Wakandarasi. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 utekelezaji wa programu ulikuwa kama ifuatavyo:-

**PROGRAMU NDOGO YA MAENDELEO YA MAKAAZI**

38. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo hii ina lengo la kuwapatia watumishi wa umma na wananchi makaazi bora pamoja na kusimamia ujenzi unaozingatia viwango.

**WAKALA WA MAJENGO ZANZIBAR**

39. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Majengo imeanzishwa kwa Tangazo la Serikali la Kisheria (Legal Notice) Namba 50 ya Mwaka

2017. Jukumu la msingi la Wakala wa Majengo ni kusimamia na kuratibu miradi ya ujenzi na matengenezo ya Majengo ya Serikali ili kuhakikisha ubora wa majengo hayo, pia ina jukumu la kutoa huduma ya makaazi kwa Viongozi wa Serikali, Maafisa Wakuu Wandamizi wa Serikali na Watumishi wa Umma.

**40.** **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Majengo kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022 iliendelea kutekeleza kazi zake kama inavyonekana katika ukurasa wa 28 hadi 29 wa hotuba yangu.

**41.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wakala wa Majengo ilipangiwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 250.** Hadi kufikia Machi, 2022 jumla ya **TZS milioni 139.746** zimekusanywa ambazo sawa na **asilimia 56** ya makadirio.

Kwa upande wa matumizi Wakala wa Majengo ilipangiwa ruzuku ya **TZS Milioni 350.0** kwa kazi za kawaida, hadi kufikia Machi, 2022 jumla ya **TZS Milioni 62.950**

zimetumika ambazo sawa na **asilimia 18** na **asilima 26** ya ulinganisho wa fedha zilizopangwa kwa miezi tisa (9).

**SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR**

42. **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Nyumba Zanzibar ni taasisi inayojitegemea iliyoanzishwa kwa Sheria namba 6 ya mwaka 2014. Taasisi hii imepewa Mamlaka ya kusimamia na kuendeleza sekta ya nyumba Zanzibar kwa lengo la kuongeza pato la taifa na kuwapatia wananchi makaazi bora na salama pamoja na kuziimarisha nyumba za Shirika zilizopo.

43. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Shirika la Nyumba kupitia Programu hii ndogo imetekeleza kazi zake kama zinazovyoonekana katika ukurasa wa 31 na 32 ya hotuba yangu.

44. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa Fedha 2021/22 Shirika la Nyumba lilitarajia kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 3.050** kutokana na kodi za nyumba, mikataba,

dhamana, adhabu na nyenginezo ambapo hadi kufikia Machi, 2022 jumla ya **TZS Bilioni 3.409** zimekusanywa kutoka katika vyanzo hivyo sawa na **asilimia 112** ya makadirio.

Kwa upande wa matumizi, Shirika lilikadiria kutumia jumla ya **TZS Bilioni 3.658** kwa kazi zake mbali mbali ambapo hadi kufikia Machi, 2022 jumla ya **TZS Bilioni 2.066** zimetumika sawa na **asilimia 56** ya makadirio.

**BODI YA KONDOMINIO**

**45. Mheshimiwa Spika,** Bodi hii imeanzishwa kwa Sheria ya Kondominio namba 10 ya mwaka 2010 ambayo imetokana na Sera ya nyumba ya mwaka 2008. Majukumu ya msingi ya Bodi ni kusajili, kuratibu na kusimamia matumizi ya pamoja kwa majengo yenye sehemu zinazomilikiwa na mtu zaidi ya mmoja.

**46. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 Bodi ya

Kondominio imefanikiwa kutekeleza kazi zake kama inavyoonekana katika ukurasa wa 33 hadi wa 34 wa hotuba yangu.

47. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2021/2022 Bodi ya Kondominio ilikadiria kukusanya jumla ya **TZS Milioni 137.347** hadi kufikia Machi, 2022 jumla ya **TZS Milioni 381.749** ambazo ni sawa na asilimia 278 ya makadirio.

Kwa upande wa matumizi Bodi ya Kondominio ilipangiwa ruzuku ya **TZS milioni 234** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake. Hadi kufikia Machi, 2022 fedha zilizoingizwa ni **TZS Milioni 51.0** ambazo ni sawa asilimia 22 na **asilimia 29** kwa ulinganisho wa fedha zilizopangwa kwa miezi tisa (9).

## BODI YA KUDHIBITI KODI ZA NYUMBA

48. **Mheshimiwa Spika,** Bodi ya kudhibiti kodi za Nyumba imeanzishwa kwa Sheria ya kudhibiti kodi za Nyumba, Sura ya 98 ya mwaka 1953 (Cap. 98 of 1953). Majukumu

ya Msingi ya Bodi hii ni kusikiliza na kuzitolea maamuzi kesi zinazotokana na migogoro ya upangishaji wa Nyumba za Serikali na Nyumba binafsi.

49. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba imetekeleza kazi zake kama inavyoonekana katika ukurasa wa 35 wa hotuba yangu.

50. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba imepangiwa ruzuku ya **TZS Milioni 130.0** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi, 2022 fedha zilizopatikana ni **TZS Milioni 40.0** ambazo sawa na **asilimia 30.77** na **asilimia 38.9** kwa ulinganisho wa fedha zilizopangwa kwa miezi tisa (9).

## BODI YA USAJILI WASANIFU WAHANDISI NA WAKADIRIAJI MAJENGO

51. **Mheshimiwa Spika,** Bodi hii imeanzishwa kwa Sheria ya Usajili wa Wasanifu,

Wahandisi na Wakadiriaji Majengo namba 5 ya Mwaka 2008. Majukumu ya msingi ya Bodi hii ni kusimamia, kudhibiti na kuwaendeleza Wataalamu wa ujenzi ili waweze kufanya kazi zao kwa utaalamu na viwango vinavyotakiwa.

52. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiraji Majengo imetekeleza kazi zake kama zinavyoonekana katika ukurasa wa 36 wa hotuba yangu.

53. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo ilipangiwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 417.012.** Hadi kufikia Machi, 2022 jumla ya **TZS Milioni 231.316** zimekusanywa ambazo sawa na asilimia 55.5 ya makadirio.

Kwa upande wa Matumizi Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo imepangiwa ruzuku ya **TZS Milioni 631.800** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi,

2022 fedha zilizopatikana ni **TZS Milioni 68.0** ambazo sawa na **asilimia 10.7** na **asilimia 16.1%** kwa ulinganisho wa fedha zilizopangwa kwa miezi tisa (9).

## BODI YA USAJILI WAKANDARASI

54. **Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Usajili wa Wakandarasi imeanzishwa kwa Sheria ya Usajili wa Wakandarasi namba 6 ya mwaka 2008. Majukumu ya msingi ya Bodi hii ni kusimamia Kampuni za ujenzi na miradi ya ujenzi inayotekelezwa nchini ili kuzingatia viwango na usalama.

55. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 Bodi ya Usajili Wakandarasi imetekeleza kazi zake kama inavyoonekana katika ukurasa wa 37 hadi wa 38 wa hotuba yangu.

56. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Bodi ya Wakandarasi ilipangiwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 801.814.** Hadi kufikia Machi, 2022 jumla ya **TZS milioni 502.101** zimekusanywa ambazo sawa na **asilimia 63** ya makadirio.

Kwa Upande wa Matumizi Bodi ya Wakandarasi imepangiwa ruzuku ya **TZS Milioni 263.200** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi, 2022 fedha zilizopatikana ni **TZS Milioni 68.00** ambazo sawa na **asilimia 26** na **asilimia 37.1** kwa ulinganisho wa fedha zilizopangwa kwa miezi tisa (9).

## MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEEO YA MAKAAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

57. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wizara yangu ilipangiwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 1.294** kutokana na vyanzo mbali mbali vya Taasisi zake. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2022 jumla ya **TZS Bilioni 1.553** zimekusanywa. Kiwango hichi ni sawa na **asilimia 120** ya makadirio. Kwa ufafanuzi zaidi **naomba angalia Kiambatisho "B"**.

58. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara yangu imepangiwa kutumia jumla

ya **TZS Bilioni 19.117.** Kati ya Fedha hizo, **TZS Bilioni 8.8074** ni kwa ajili ya kazi za kawaida na mishahara na **TZS Bilioni 10.310** kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2022 Wizara yangu ilikwishapatiwa **TZS Bilioni 4.392** kwa kazi za kawaida na mishahara sawa na **asilimia 50** na kwa kazi za Maendeleo hakuna fedha iliyopatikana hadi Machi, 2022. Hivyo kufanya jumla ya fedha zote tulizozipata kuwa ni **TZS Bilioni 4.392** sawa na **asilimia 23** ya makadirio. Kwa ufafanuzi zaidi **angalia kiambatisho“C”**

## MWELEKEO WA MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

59. **Mheshimiwa Spika,** baada ya kutoa maelezo ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara yangu kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, sasa naomba kuwasilisha mwelekeo wa Bajeti yenye kuzingatia Programu ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

60. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi imepangiwa kutumia jumla ya **TZS Bilioni 26. 942** kati ya hizo **TZS Bilioni 5.725** ni kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida kwa fungu la Wizara, kati ya fedha hizo jumla ya **TZS Bilioni 2.558** zimetengwa kwa ajili ya mishahara kwa Idara zilizo chini ya Wizara, **TZS Bilioni 1.183** kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya uendeshaji wa ofisi kwa Idara zilizo chini ya Wizara na **TZS Bilioni 1.984** ni ruzuku kwa ajili ya Taasisi za Wizara na **TZS Billioni 17.0** kwa ajili ya kazi za Maendeleo. Vilevile, Jumla ya **TZS Bilioni 4.216** kwa kazi za kawaida na mishahara kwa ajili ya fungu la Kamisheni ya Ardhi.

61. **Mheshimiwa Spika,** aidha, kwa mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi imepangiwa kukusanya mapato ya jumla ya **TZS Bilioni 2.922** zinazoingia katika mfuko Mkuu wa Serikali, kati ya fedha hizo Jumla ya **TZS Bilioni 1.900** kwa ajili ya makusanyo yanayotokana na vyanzo vya fungu la

Wizara na jumla ya **TZS Bilioni 1.022** kwa ajili ya makusanyo yanayotokana na vyanzo vya Fungu la Kamisheni ya Ardhi. Kwa ufafanuzi zaidi **angalia viambatisho vya D1 – D4**

**62. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka huu wa fedha imejipangia kutekeleza bajeti yake kwa kuzingatia vipaombele vifuatavyo:-

i. Kufanya utambuzi wa maeneo ya Unguja na Pemba ili kupunguza Migogoro ya ardhi nchini.
ii. Kuandaa Mipango ya matumizi ya ardhi ya miji mbalimbali (Local Area Development Plans) kwa Unguja na Pemba kwa ajili ya kudhibiti ujenzi holela.
iii. Kufanya matengenezo ya nyumba za Maendeleo na zisizokuwa za Maendeleo kwa Upande wa Unguja na Pemba ili ziwe imara na kuwa katika mazingira mazuri zaidi.

**63. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi itatekeleza

vipaombele hivyo kupitia Programu Kuu tatu kama ifuatavyo: -

a. **Programu PN0201:** Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo Makaazi
b. **Programu PN0202:** Usimamizi wa Ardhi
c. **Programu PN0203:** Maendeleo ya Makaazi

64. **Mheshimiwa Spika,** naomba sasa uniruhusu kutoa maelezo kuhusu Programu Kuu na Programu ndogo za Wizara yangu kama ifuatavyo:-

**PROGRAMU KUU PN0201: UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI**

65. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inajukumu la kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Kazi za Wizara ambapo matokeo ya muda mrefu yanayotarajiwa ni kukuza ufanisi katika utawala wa rasilimali Ardhi na huduma za Makaazi kwa jamii. Programu hii itasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Uendeshaji na Utumishi, na Afisi Kuu

Pemba ambapo jumla ya **TZS Bilioni 3.157** zinatarajiwa kutumika katika utekelezaji wake. Programu hii imegawika katika Programu ndogo kama ifuatavyo:-

a. **Programu ndogo SN020101:**Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti
b. **Programu ndogo SN020102:**Utawala na Uendeshaji
c. **Programu ndogo SN020103:** Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba

**PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA MIPANGO, SERA NA UTAFITI**

66. **Mheshimiwa Spika,** dhumuni la Programu ndogo hii ni uratibu wa shughuli za kazi za Wizara kwa Ufanisi. Kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Programu hii imepanga kukamilisha mapitio ya Sheria zinazohusu matumizi ya ardhi, na kuandaa Sera ya Nyumba na Sera ya Mipango Miji, kuratibu mapitio ya Sheria zote zilizo chini ya Taasisi za Wizara, Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya Wizara, kufanya Tafiti kwa ajili ya kuwezesha utoaji

wa huduma bora katika Sekta za Wizara na Kuratibu Vikao vya Ushirikiano baina ya Taasisi za SMZ na SMT.

67. **Mheshimiwa Spika,** vilevile, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara Kupitia Proramu hii imepanga kuratibu utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Sekta ya Ardhi na Makaazi inayohusisha Mradi wa Matengenezo ya Nyumba za Maendeleo na Mradi wa Utayarishaji wa Mpango wa Matumizi ya Ardhi.

68. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Programu hii kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS Milioni 335.270** kwa ajili ya kazi za kawaida na mishahara, ambapo **TZS Milioni 184.0** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **TZS Milioni 151.270** kwa ajili ya Mishahara.

## PROGRAMU NDOGO YA UTAWALA NA UENDESHAJI

69. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 programu hii imepanga kuendeleza utoaji wa huduma za uendeshaji na usimamizi wa rasilimali za Wizara, kuwajengea uwezo wafanyakazi na kuwapatia stahiki zao kwa mujibu wa taratibu za Utumishi, kuhakikisha kuwepo kwa watendaji wa kutosha na wenye sifa, kufanya mapitio ya mkataba wa huduma kwa wateja, kuratibu mapitio ya miundo na majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Wizara ili kuleta ufanisi zaidi katika utekelezaji wa kazi na kuimarisha ushirikiano baina ya Wizara.

70. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Programu hii kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS Bilioni 2.0748** kwa ajili ya kazi za kawaida na mishahara, ambapo **TZS Milioni 491** kwa ajili ya kazi za Kawaida na **TZS Bilioni 1.583** kwa ajili ya Mishahara.

## PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA SHUGHULI ZA WIZARA PEMBA

71. **Mheshimiwa Spika,** dhumuni la Programu hii ni Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba, ambapo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Programu hii imepanga kuratibu shughuli za Wizara kwa upande wa Pemba, kuimarisha kazi za usimamizi na ufuatiliaji wa Programu na miradi ya Maendeleo ya Wizara Pemba pamoja na Kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi kwa wafanyakazi wote .

72. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Programu hii kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2022/2023, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS Milioni 747.600** kwa ajili ya kazi za kawaida na mishahara, ambapo **TZS Milioni 182** kwa ajili ya kazi za kawaida na **TZS Milioni 565.600** kwa ajili ya mishahara.

## PROGRAMU KUU PN0202: USIMAMIZI WA ARDHI

**73. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina jukumu la kuhakikisha usalama wa matumizi na umiliki wa ardhi (Security of Land Tenure). Matokeo ya muda mrefu yanayotarajiwa ni kuwa na matumizi ya ardhi yaliyo bora Kiuchumi na Kijamii. Programu hii inasimamiwa na Kamisheni ya Ardhi, Bodi ya Uhaulishaji Ardhi, Afisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali na Mahakama ya Ardhi.

**74. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina Programu ndogo ifuatayo:-

### PROGRAMU NDOGO YA USIMAMIZI WA ARDHI

**75. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/2023 Programu hii ililenga kutekeleza shughuli zote zinazohusiana na masuala ya Ardhi na inatekelezwa na Taasisi zifuatazo: -

## MAHAKAMA YA ARDHI

76. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Mahakama ya Ardhi kupitia programu hii ndogo imepanga kuendelea na kusikiliza na kutoa maamuzi ya kesi za migogoro ya ardhi, kutoa elimu na kufanya matengenezo ya majengo yake.

## KAMISHENI YA ARDHI

77. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kupitia Kamisheni ya Ardhi, imepanga kutekeleza Mradi wa Mpango wa Matumizi ya Ardhi Zanzibar, ugawaji na usimamizi wa ardhi, kuratibu na kusimamia usajili wa ardhi, upimaji na utoaji wa ramani za ardhi pamoja na upangaji wa miji na matumizi bora ya ardhi. Maelezo zaidi ya malengo hayo yanapatikana katika ukurasa wa 48 hadi wa 49 wa hotuba yangu.

## BODI YA UHAULISHAJI ARDHI

78. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/2023 Bodi ya Uhaulishaji imepanga kutekeleza kazi zake za usimamiaji wa Uhaulishaji wa Ardhi, kutoa elimu kwa jamii na kuimarisha mfumo wa uwekaji kumbukumbu za uhaulishaji wa ardhi nchini.

79. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Kamisheni ya Ardhi (COLA) imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 1.022** kutokana na vyanzo vyake mbalimbali vya mapato. Aidha, Kamisheni ya Ardhi imepangiwa kutumia jumla ya **TZS Bilioni 4.216** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida, mishahara pamoja na ruzuku kwa Bodi ya Uhaulishaji.

## OFISI YA MTHAMINI MKUU WA SERIKALI

80. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali imepanga kutekeleza kazi ya uidhinishaji wa ripoti za

uthamini,kuwasajili na kuwapatia leseni Wathamini, Kutayarisha kanuni ya viwango vya thamani ya Ujenzi na Ardhi pamoja na muongozo wa uthamini wa fidia na kutoa elimu kwa jamii.

81. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Programu ya Usimamizi wa Ardhi kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS Bilioni 1.746** zinatarajiwa kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida na Maendeleo, ambapo **TZS Milioni 488.400** kwa ajili ya kazi za kawaida, **TZS Milioni 258** kwa ajili ya Mshahara wa Mahakama ya Ardhi na **TZS Bilioni 1.00** kwa ajili ya kazi za Maendeleo.

**PROGRAMU KUU PN0203: MAENDELEO YA MAKAAZI**

82. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina jukumu la kuimarisha Makaazi bora na salama kwa kuanzisha na kuendeleza miji ya kisasa pamoja na usimamizi wa shughuli

za ujenzi Nchini. Matokeo ya muda mrefu yanayotarajiwa ni kuwepo kwa makaazi bora na kuimarika kwa miji yetu. Programu hii inasimamiwa na Wakala wa Majengo, Shirika la Nyumba, Bodi ya Kondominio, Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba, Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo na Bodi ya Usajili Wakandarasi.

**PROGRAMU NDOGO YA MAENDELEO YA MAKAAZI**

83. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa makaazi salama na endelevu kwa wananchi na watumishi wa ngazi zote wa Serikali, pamoja na kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji wa sekta binafsi katika huduma ya makaazi.

**WAKALA WA MAJENGO**

84. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wakala wa Majengo imepanga kutekeleza kazi ya utoaji huduma za ushauri wa miradi kwa taasisi, huduma

za ujenzi wa miradi mbalimbali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na usimamizi wa Majengo ya Serikali.

## SHIRIKA LA NYUMBA

85. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Shirika la Nyumba kupitia Programu hii ndogo imepanga kuengeza kasi ya utoaji huduma nzuri kwa jamii kwa kufanya matengenezo ya nyumba za Shirika pamoja na ujenzi wa majengo mapya ya maakaazi na biashara.

## BODI YA KONDOMINIO

86. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Bodi ya Kondominio imepanga kutekeleza kazi za usajili wa Kondominio kwa miradi mbalimbali, kusimamia Jumuiya za Kondominio na kutoa elimu kwa jamii.

## BODI YA KUDHIBITI KODI ZA NYUMBA

87. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba imepanga kuendelea na kusikiliza na kutoa maamuzi ya kesi za migogoro ya kodi za nyumba pamoja na kutoa elimu kwa jamii.

## BODI YA USAJILI WASANIFU WAHANDISI NA WAKADIRIAJI MAJENGO

88. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Bodi ya Usajili Wasanifu Wahandisi na Wakadiraji Majengo imepanga kuendelea na usajili wa Wataalamu wa fani za ujenzi wa majengo, Mafundi sanifu na Makampuni ya ushauri wa ujenzi, kufanya ukaguzi wa kazi za ujenzi wa Majengo na kutoa mafunzo kwa wahitimu wa fani za ujenzi.

## BODI YA USAJILI WA WAKANDARASI

89. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Bodi ya Usajili

Wakandarasi imepanga kuendelea na usajili wa Wakandarasi pamoja na miradi ya Wakandarasi, usimamizi wa ujenzi wa miradi ya Wakandarasi pamoja na uhamasishaji wa wanafunzi kusoma masomo ya Sayansi ili kupata Wataalamu wazuri wa fani za ujenzi.

90. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Programu ya Maendeleo ya Makaazi kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS Bilioni 17.821** kwa ajili ya kazi za kawaida na Maendeleo ambapo **TZS Bilioni 1.821** ni kwa ajili ya ruzuku na **TZS Bilioni 16.0** kwa ajili ya kazi za Maendelo.

## SHUKURANI

91. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua fursa hii kwa mara nyengine tena kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia fursa na uwezo wa kuisoma hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

92. **Mheshimiwa Spika,** naomba uniruhusu kumshukuru tena Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwa imani yake tena kwangu na kunipa nafasi hii muhimu ya kuitumikia Nchi yangu kupitia Wizara hii, nami naahidi nitajitahidi kadri ya uwezo wangu kumsaidia kwa uwezo wangu wote. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais kwa maelekezo yao wanayonipatia. Wote nawaombea kwa Mwenyezi Mungu awazidishie busara, uadilifu, afya njema na maisha marefu pamoja na familia zao.

93. **Mheshimiwa Spika,** kwa mara nyengine tena naomba kukushukuru wewe mwenyewe, Naibu Spika na Waheshimiwa wote kwa kunisikiliza kwa utulivu na kwa umakini mkubwa wakati nikisoma hotuba ya Wizara yangu.

94. **Mheshimiwa Spika,** naomba pia kuwashukuru Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Baraza la

Wawakilishi zilizotembelea na kufanya vikao na Wizara yangu. Maoni, ushauri na maelekezo yao kwetu yamesaidia sana sio tu katika utekelezaji wa kazi za Wizara bali pia katika utayarishaji wa Hotuba hii. Shukurani maalumu kwa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa msaada na Ushirikiano wao mkubwa waliotupatia.

95. **Mheshimiwa Spika,** shukurani maalumu ziwaendee Uongozi na wafanyakazi wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Unguja na Pemba kwa Ushirikiano wao mkubwa kwangu, namuomba Mwenyezi Mungu awajaalie wote afya njema na maisha marefu yenye kheri. Naamini Ushirikiano huo utaendelea ili tuweze kuendelea kutoa huduma bora kwa Wananchi. Kipekee naomba nimshukuru Mheshimiwa Riziki Pembe Juma, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kunikabidhi Wizara hii ikiwa katika utekelezaji mzuri.

96. **Mheshimiwa Spika,** pia nachukua fursa hii kuwashukuru Wadau mbalimbali wa

Serikali na wasio wa Serikali wakiwemo Milele Foundation, Property International pamoja na Wananchi kwa ujumla kwa ushirikiano mkubwa kwa Wizara yangu kuhakikisha kuwa majukumu tuliopewa yanatekelezwa kama yalivyokusudiwa na kwa ufanisi mkubwa.

97. **Mheshimiwa Spika,** na mwaka ujao wa Fedha 2022/2023, Wananchi wategemee ongezeko kubwa la ubora wa huduma na ufanisi katika utendaji wa kazi za Wizara yangu, licha ya changamoto kubwa ya migogoro ya ardhi ya muda mrefu inayoendelea. Wizara itahakikisha usimamizi wa ardhi, utatuzi wa migogoro ya ardhi na udhibiti wa ujenzi utakuwa bora zaidi kutokana na mikakati iliyowekwa sambamba na kuimarisha Miji yetu kwa ujenzi wa nyumba za kisasa.

98. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee, napenda kuishukuru familia yangu kwa ustahamilivu, subra na ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kutekeleza majukumu niliokabidhiwa. Na kwa upekee

nawashukuru Kinamama wa Mkoa wa Kusini Unguja kwa Ushirikiano wao wanaonipatia.

**MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2022/2023**

99. **Mheshimiwa Spika,** ili Wizara yangu iweze kutekeleza Programu Kuu na Programu Ndogo nilizozieleza, naliomba Baraza lako iidhinishe jumla ya fedha **TZS 26,942,270,000** kwa utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kati ya hizo **TZS 5,725,670,000** kwa kazi za kawaida, mishahara na ruzuku kwa Taasisi zilizochini ya fungu la Wizara na **TZS 17,000,000,000** kwa kazi za Maendeleo, pamoja na Jumla ya **TZS 4,216,600,000** kwa kazi za kawaida, mishahara na ruzuku kwa ajili ya fungu la Kamisheni ya Ardhi.

100. **Mheshimiwa Spika,** pia naomba idhini ya kukusanya Mapato ya Fedha **TZS 2,922,815,000** kutoka vyanzo mbalimbali vya Wizara yangu, ambapo

**TZS 1,900,000,000** kutoka katika vianzio mbali mbali vilivyomo ndani ya fungu la Wizara, na **TZS 1,022,815,000** kwa ajili ya Mapato yanayotokana na vianzio mbali mbali vilivyomo ndani la Fungu la Kamisheni ya Ardhi kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kwa ufafanuzi zaidi **naomba angalia kiambatisho "D1, D2, D3 na D4".**

## HITIMISHO

101. **Mheshimiwa Spika,** nawaomba sasa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako waipokee, waijadili kwa kina, kisha watushauri na kutuelekeza na hatimae wayapitishe makadirio haya. Tuna imani kubwa kuwa michango ya waheshimiwa wajumbe itatusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu ya kazi vizuri zaidi katika kipindi kijacho cha Mwaka wa Fedha 2022/2023.

102. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**Mheshimiwa Rahma Kassim Ali (MBM)**
**Waziri wa Ardhi na Maendeleeo ya Makaazi Zanzibar.**